

# JARIDA LA JOTOARDHI



Jarida Mtandaoni | Januari - Machi, 2022 | Toleo Namba. 003

## KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI.

IMERIDHISHWA NAMAENDELEO YA MRADI WA UMEME WA NISHATI  
YA JOTOARDHIUNAOSIMAMIWA NA KAMPUNI YA JOTOARDHI TANZANIA  
(TGDC).



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania Mhandisi Kato Kabaka akitoa maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa Jotoardhi Songwe kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipofanya ziara ya kutembelea rasilimali hiyo adhimu Songwe.



@TgdcTanzania



[www.tgdc.go.tz](http://www.tgdc.go.tz)



# SALAAM ZA KWAHERI

## KUTOKA KWA MENEJA MKUU.

### Ndugu Wafanyakazi wa TGDC.

Nawasalimu; kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!!!

Tunakila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima kwa kuliendesha gurudumu la TGDC tukiwa na afya njema na furaha. Ingawa wakati ni ukuta na inaanza sekunde, dakika, saa, siku, wiki, mwezi na hatimaye mwak, lakini pia sifa zote nazipeleka kwa aliye juu na watumishi wenzangu kwa kuweza kutumikia vyema taasisi hii kwa kazi kubwa ya uaminifu na uadilifu hadi kufikia kustaaful kwangu.

Leo tarehe 31 Machi, 2022 jahazi langu limetia nanga katika utumishi wangu wa umma. Pia sina budi kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awasadie katika kutekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia weledi na kwa mujibu wa taratibu na kanuni za utumishi wa umma ili muwashe umeme wa Jotoardhi.

Kutokana na changamoto chanya na hasi zote nilizokumba na nazo katika utumishi wangu ambazo nilizichukua kama ni fursa na zilinipa nguvu ya kusukuma gurudumu hili hadi leo hii. Nakuombeni sana mchukue changamoto zote mnazokutana nazo katika majukumu yenu na mzigeuze kuwa mtaji wa kuwapeleka hatua moja mbele na si za kuwarudisha nyuma kwani TGDC ni nyie na nyie ni TGDC.

Ndugu, Wafanyakazi Naomba nichukue fursa hii pia kuwakumbusha mambo mbalimbali mnayopaswa kuyabeba kwa uzito mkubwa ili mfike safari yenu ya mafanikio, Kwa kila mmoja wenu ni lazima ajitathmini na kwa kupitia Idara zetu kwa kujiuliza ni kitu gani umechangia katika Kampuni kwani kila mmoja wetu ana umuhimu mkubwa na ndiyo maana yupo hapa ili Kampuni izidi kusonga mbele na kuipatia Taifa manufaa makubwa.

Vile vile ni muhimu kuelewa mpango mzima wa kampuni yetu inataka nini na mikakati tunayojipangia inatimizwa kwa wakati. Epukeni kazi moja kurudia mara kwa mara kwani inaiongezea Kampuni gharama kubwa. Jiwekeeni ratiba inayoleweka ya kazi zenu itasaidia kufanya kazi zote kwa wakati na kwa weledi mkubwa.

Kila mmoja wetu ni balozi wa TGDC. Lazima muwe na ari ya kuweka nguvu katika ujuzi wenu. Hii itasaidia kufikia malengo mnayojipangia kwa mafanikio makubwa sana, na wanaopewa majukumu ya kusimamia Miradi muhakikishe mnaiongeza spidi. Ni kipindi ambacho wafanyakazi pia mnatakiwa kufikiria kibiashara zaidi katika Miradi yetu kwa kuihamishia uzoefu wetu katika kutupatia pesa.



**Mhandisi Kato Kabaka  
Meneja Mkuu TGDC**

Kwa mara nyingine tena nashukuru kuwa sehemu ya TGDC ninawaahidi ntakuwa balozi wenu mzuri sana kwa ndani na nje ya nchi yetu. Na naona fahari kubwa nimeacha nyuma jeshi kubwa na makini ambalo wana ari kubwa ya kuenteleza rasilimali hii Jadidifu ya Jotoardhi na kuendeleza miradi ya moja kwa moja. Kila mmoja kwa nafasi yake afanye kinachomuhusu kwa umakini wote mpo TGDC kwa sababu hivyo muache kufanya kazi kimazoea badala yake mtumie ujuzi wenu wote na kwa wakati. Nakuombeni muwe na upendo, nidhamu kwani palipo na vitu hivyo kazi huwa ni nyepesi.



@TgdcTanzania



[www.tfdc.go.tz](http://www.tfdc.go.tz)

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI IMERIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA UMEME WA NISHATI YA JOTOARDHI UNAOSIMAMIWA NA KAMPUNI YA JOTOARDHI TANZANIA (TGDC).

Katika Mradi Songwe utafiti umekamilika, upembuzi wa kina umekamilika na uendelezaji wa matumizi ya jotoardhi unaendelea..

Tunatarajia kuanza kuzalisha megawati 5 hadi 38 za umeme.

Eng. Kato Kabaka  
Mkurugenzi Mkuu TGDC

Mwenyekiti wa Kamati amewataka watendaji kuongeza jitihada katika utekelezaji wa mradi huo ili mipango ya kampuni iliyowekwa inatekelezwa kwa wakati kadiri ya Serikali ilivyotarajia.

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania Mhandisi Kato Kabaka akitoa maelezo ya Rasilimali ya Jotoardhi Songwe kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipofanya ziara yakutembelea rasilimali hiyo adhimu Songwe.

Tuna mipango mbalimbali ya kuzalisha umeme katika nchi yetu; ili tuwe salama tumekubaliana kwamba tusitegemee chanzo kimoja tuwe na vyanzo mchanganyiko, sasa vyanzo tulivyo navyo ni pamoja na jotoardhi ambayo tunaendeleza sasa ili ifike mahali tuweze kuzalisha umeme.

Mhe. Dunstan Kitandula  
mwenyekiti kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini



Akizungumza katika eneo la Mradi huo Kijiji cha Nanyala wilayani Mbozi, mwenyekiti wa kamati hiyo Mheshimiwa Dunstan Kitandula ameipongeza TGDC kwa kazi nzuri huku akiwataka kuendelea kuwa wabunifu ili kuwafungua macho wa Tanzania kuziona fursa kupitia uwekezaji huo.



@TgdcTanzania



# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI IMERIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA UMEME WA NISHATI YA JOTOARDHI UNAOSIMAMIWA NA KAMPUNI YA JOTOARDHI TANZANIA (TGDC).



“ Nichukue fursa hii ku-wapongeza sana Kampuni ya TGDC kwa jitihada hizi wanzaofanya waendelee na ubunifu wanaoufanya ili kuwafunga macho wananzania waone fursa zinazoweza kuji-tokeza kupitia sekta hii.

**Mhe. Dunstan Kitandula**  
Mwenyekiti Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mwenyekiti wa Kamati amewataka watendaji kuongeza jitihada katika utekelezaji wa mradi huo ili mipango ya kampuni iliyowekwa inatakelezwa kwa wakati kadiri ya Serikali ilivyotarajia.

Alipongeza kwa ushirikiano kampuni iliyou-fikia kwa jamii inayozunguka mradi na uongozi wa mkoa kwa ujumla, huku akiomba kuendeleza jitihadi zaidi za kushirikisha wadau mbalimbali katika miradi ya jotoardhi.

Ameongeza kuwa; "Serikali imeanza kuwekeza kwenye eneo hili na maeneo mengine mengi nchini kwa manufaa ya Taifa na kwamba umeme wa nishati ya jotoardhi una faida kubwa kwani ni rafiki wa mazingira, ni wa bei nafuu na unapati-kani kipindi chote hauna masika wala kiangazi hivyo tunaenda kuishauri Serikali tuwekeze nguvu Zaidi katika rasilimali hii'ma hizo kwa umbali mrefu



**KAMATI YA NISHATI NA  
MADINI YAPIGIA CHEPUO  
UENDELEZAJI JOTOARDHI**

# KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

**WAFANYAKAZI WANAWAKE KUTOKA**

**TGDC, ETDCO NA TCPM**

**WAWASHIKA MKONO WATOTO WANAOGUA SARATANI**

Ilikuwa ni siku ya maadhimisho yaSiku ya Wanawake, wafanyakazi wanawake kutoka Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) kwa kushirikiana na Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme (ETDCO) pamoja na Kampuni ya Uzalishaji wa Nguzo za Zege (TCPM) ambazo zote ziko chini ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Machi 05, 2022 wametembelea hostel ya watoto wanaougua ugonjwa wa saratani jijini Dar es Salaam na kukabidhi msaada wa mahitaji muhimu.

Msaada huo wa mahitaji muhimu uliokabidhiwa kwa watoto hao, ni pamoja na dawa, vifaa tiba, vyakula, vifaa vya kufanya usafi mbavyo kwa pamoja vimegharimuki cha shilingi milioni tatu (3,000,000).

Akiongea baada ya kukabidhi msaada huo, Me neja Rasilimali watu na Utawala wa TGDC, Bi. Judith S. Gowele amesema, katika kushereheke siku ya wanawake, wao kama wafanyakazi wanawake hujumuika pamoja na watu wenye uhitaji na kwa mwaka huu wameona wajumuike na watoto wanaougua saratani na kuwapa mahitaji muhimu.

Ameongeza kuwa, kwa kufanya hivyo, ni kuonesha ishara ya upendo, kujali na uthamini si kwa watoto tu, hata kwa wazazi, walezi na wahudumu wa afya wanaowahudumia watoto hao.

"Katika kushereheke siku ya wanawake tumeona ni fahari kwetu kujumuika na watoto wanaougua saratani, kuendelea kuwaonesha upendo, kuwathamini na kuwajali ili waendelee kujiona ni sehemu ya jamii sawa na wengine" alisema Bi. Gowele.

Bi Gowele ametumia fursa hiyo kuwataka wazazi na walezi wa watoto hao kutokata tamaa, kuwa na imani na kuendelea kumuomba Mungu kwani Changamotohiyo inaweza kumkuta mtoto ye yeyote na mzazi ye yeyote. Kwa upande wake, mtaalamu wa Taarifa za kijiografia (GIS) kutoka TGDC, Bi. Anastacia Ndimbo, amesema kuwa; kitendo cha kukaa hospitali wiki, mwezi au mwaka ni gharama kubwa sana



kwani kuna utaratibu mwingine wa maisha unasima ma, na hivyo ametoa rai kwa makundi mengine kuji tokeza kusaidia wenye uhitaji hospitalini ikiwemo watoto hao.

"Kukaa hospitali wiki, mwezi ni gharama sana na inaumiza, mbali na kukabidhi misaada yetu, nitoe rai kwa mtu mmoja mmoja na makundi ya kijamii pamoja na taasisi kujitokeza kusaidia watu wenye uhitaji na hio ni moyo wa upendo sawa na maandiko katika vitabu vya dini" alisema Bi. Ndimbo Hostel ya watoto wanaougua ugonjwa wa saratani jijini Dar es Salaam inawahudumia watoto zaidi ya 800 kwa mwaka kutoka mikoa yote kote nchini, ambapo wafanyakazi hao wametoa wito kwa taasisi na makundi mengine ya kijamii kujitokeza kuwasaidia.

Wakati huo huo Afisa Mkuu wa Fedha, CPA Renatha Ndege kutoka Kampuni Mama TANESCO ambaye alijumuika na timu ya Wanawake wa TGDC katika chakula Cha mchana katika Mgahawa wa Karambezi alisisitiza "nidhamu katika kazi kwa watu wote ndiyo msingi wa chachu ya ukuaji kwamtum mmoja mmoja na Kampuni kwa ujumla"

Maadhimisho ya siku ya Wanawake duniani yalianzishwa mwaka 1908 na kwa sasa yanaadhimishwa kwa mwaka wa 101, ambapo kitaifa siku ya Wanawake Duniani iliadhimishwa Machi 08, katika ukumbi wa mikutano Mlimani City jijini Dar es Salaam huku kauli mbiu yake ikiwa ni "Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu"



# KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

WAFANYAKAZI WANAWAKE KUTOKA TGDC KATIKA KUADHIMISHA  
SIKU YA WANAWAKE KITAIFA



Wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) wakiwa katika picha ya pamoja katika fukwe za bahari ya hindi katika Mgahawa wa Kalambezi, Masaki.



Wafanyakazi wa TGDC wakiwa wameshika bango  
lililobeba ujumbe wa maadhimisho ya siku ya  
Wananwake Duniani machi 08,  
katika Uwanja wa Uhuru Jijini Dar es salaam.

Wafanyakazi wanawake wa Kampuni Tanzu za  
TANESCO wakiwa na nyuso za furaha katika kilele  
chasiku ya Wanawake Duniani Machi 08, katika Uwanja  
wa Uhuru Jijini Dar es salaam.



@TgdcTanzania



**HABARI PICHA:**

**ZIARA YA KAMATI YA KUDUMU  
YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI  
MKOANI SONGWE**



@TgdcTanzania



[www.tgdc.go.tz](http://www.tgdc.go.tz)



Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Makamba Machi 30, 2022 Jijini Dar es salaam katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati ameahidi kuisemea na kuisimamia Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania TGDC kuhakikisha lengo la Serikali linatimia la kupatikana kwa Rasilimali ya Jotoardhi hapa nchini.

Katika kikao hicho Mheshimiwa Waziri Makamba ameipongeza TGDC kwa kuitembelea ofisi yake na kujadiliana mambo mengi yenye tija kuhakikisha Kampuni inasogea mbele Zaidi kwa kutimiza majukumu yake; "Nimefurahi kuelewa Jotoardhi (Geothermal) kabla sijaingia Wizara hii nlikuwa na uelewa nayo lakini kwa sasa uelewa umekuwa mpaka na lazima nikiri kwa sasa tunaweka nguvu kubwa katika Rasilimali hii muhimu ya Jotoardhi kwani ni nishati nafuu, salama na Rafiki wa Mazingira, na popote ntakapoenda Duniani ntaenda kuizungumzia kwani ni muhimu sana".

Mheshimiwa Makamba aliongea hayo baada ya Meneja Mkuu wa TGDC anayemaliza muda wake Mhandisi Kato Kabaka kuenda kuagana naye na kumkumbushia baadhi ya mambo kama kuendeshea shughuli za Jotoardhi hasa kipindi ambacho Kampuni

inategemea kupokea mtambo wake pekee wa kuchoronga (Drilling Rig) utakaowasili mwezi Julai mwaka huu wa 2022.

"Mwezi Novemba mwaka huu kutakuwa na mkutano wa Kikanda (ARGEON - C9) kuanzia tarehe 1 -6 nchini Djibouti na kwa umuhimu wake Mheshimiwa Waziri Makamba naomba uwe sehemu ya mkutano huo amba ni fursa kubwa ya kupaza sauti kuhusu rasilimali Jadidifu ya Jotoardhi" Alisema Meneja Mkuu Mhandisi Kato Kabaka.

"Serikali yetu ni sikivu na itachukua hatua zote kuhakikisha tutahudhuria mkutano huo wa Novemba 2022, nchini Djibouti na Kuomba kuwa mwenyeji wa Mkutano ujao mwaka 2024". Alisema Waziri wa Nishati Mheshimiwa Makamba.

Katika majumuisho ya kikao hicho Mheshimiwa Waziri Makamba alimuhakikishia Meneja Mkuu anayemaliza muda wake Mhandisi Kato Kabaka kuwa tuna deni kubwa kwake na ili kulilipa ategemei kupatikana kwa matokeo mazuri TGDC. Na pia asijiweke mbali sana bado tunahitaji busara zake na akiona fursa yoyote nzuri kuhusu Jotoardhi milango yake ipo wazi akamshauri.

# MKURUGENZI MTENDAJI WA TANESCO ATEMBELEA

## KAMPUNI YA UENDELEZAJI JOTOARDHI TANZANIA (TGDC)

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Ndugu Maharage Chande amefanya ziara februari 22, 2022 katika ofisi za Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) iliyopo Msasani jijini, Dar es salaam.

Madhumuni ya ziara hiyo yalikuwa kufahamu mustakabali wa Kampuni ya TGDC katika Nyanja mbalimbali kama fedha, maendeleo ya miradi inayoendelea pamoja na njia za mawasiliano zinazotumika kuwasiliana na Kampuni kuu ambayo ni TANESCO.

Katika Salamu zake za ukaribisho kwa Mkurugenzi huyo, Meneja Mkuu wa TGDC Mhandisi Kato Kabaka alishukuru kwa ujio wake na kusema safari hiyo ni ya matumaini kwa Uendelezaji wa Jotoardhi katika taasisi yetu.

‘Jotoardhi ni mradi wa Kimkakati na hivyo ni lazima uendelee kwa kasi kwani kama nchi tupo nyuma kwenye uzalishaji wa umeme ukilinganisha na nchi nyingine na idadi ya watu tulionao, nchi kama Uturuki na Egypt zimetupita sana na sasa ni wakati wa nishati itokanayo na Jotoardhi iongeze idadi ya megawati katika gridi yetu’ alisema Maharage.

Aliongeza kuwa Jotoardhi ni mkombozi wa nishati ya umeme kwasababu chanzo cha nishati hiyo ambayo ni joto halilipiwi ni umeme nafuu, salama na rafiki wa mazingira.



**Maharage Chande  
Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO**

Umeme huo ambao hauna masika wala kiangazi unapatikana mwaka mzima hivyo ni lazima kwa TGDC kuongeza ari na jitihada kubwa kupata nishati hiyo kwani tafiti nyingi zimekwishafanyika.

Maharage alisema ni matamanio yake baada ya muda mfupi ujao TGDC itajitegemea ili kuongeza ufanisi katika kazi kwa kuandaa mkakati mzuri wa kibiashara kwani soko la uhakika la kuuza bidhaa ya umeme huo lipo na ni TANESCO, na kuelekeza kuangalia fursa zingine katika taasisi mbalimbali za uwekezajia ambao wapo na nia ya kuwekeza katika nishati ya Jotoardhi.

Naye Mhandisi Mathew Mwangomba ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ufundi amemhakikishia Mkurugenzi wa TANESCO kuifanyia kazi miradi yote ya kimkakati na kuhimiza wafanyakazi kufanya kazi miradi yote ili ikamilike kwa wakati.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Biashara Mhandisi Shakiru Idrissa ameomba Mkurugenzi Mtendaji kusaidia Sheria ya Jotoardhi kupatikana kwani itafungua njia na kuifanya kampuni hiyo kuaminika katika kutafuta mitaji na wawekezaji.

Ziara hiyo ilikamilishwa kwa Meneja Mkuu wa TGDC Mhandisi Kato Kabaka kumshukuru kwa kuwatemelea na kumuahidi kutekeleza yale yote aliyoyaagiza ili kufanikisha azma ya serikali ya kutumia nishati ya jotoardhi kama chanzo mbadala cha kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.





*Kwa mawasiliano zaid;*

**TANZANIA GEOTHERMAL DEVELOPMENT  
COMPANY LIMITED**

P. O. Box 14801,

House No. 25. Ursino, Mwai Kibaki Road,  
Dar es Salaam, Tanzania.

Tel: +255 687 833 855,

[info@tgdc.go.tz](mailto:info@tgdc.go.tz)

[www.tgdc.co.tz](http://www.tgdc.co.tz)



@TgdcTanzania



[www.tgdc.go.tz](http://www.tgdc.go.tz)